JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO
YA UFUNDI STADI
CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI SATDI CHA WILAYA YA KWIMBA

Unapojibu tafadhali taja, 05 Disemba, 2024

Kumb. Na. VETA/KWB/DVTC/UF.I/0001

…….
……
…….

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI CHUO CHA KWIMBA DVTC - HATUA YA KWANZA.

Maelezo haya yasomwe kwa umakini na Mzazi/Mlezi na Mwanafunzi.

1. Unafahamishwa kwamba umechaguliwa kujiunga na chuo tajwa hapo juu katika Fani ya _____, ngazi ya kwanza **(Level I**) kwa masomo ya BWENI/KUTWA (Boarding/Day). ……

2. Mafunzo yatachukua muda wa miaka miwili (kuanzia mwezi Januaari, 2025 mpaka Desemba 2026

3. Chuo kitafunguliwa rasmi tarehe 15/01/2025.

4. Unatakiwa kuthibitishwa na daktari wa serikali kuwa unayo afya nzuri ya kumudu mafunzo katika fani uliyopangiwa. Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical Examination Form) imeambatanishwa.

5. Unatakiwa kuthibitisha wewe mwenyewe na mzazi/mlezi/mdhamini wako kwamba unakubali nafasi ya mafunzo uliyopangiwa.

6. Unatakiwa kufuata sheria na taratibu zote za chuo zilizoambatanishwa kwenye barua.

7. Unatakiwa kufika chuoni na barua hii siku ya kuanza mafunzo.

8. Unatakiwa kununua vifaa vilivyoambatanishwa na barua hii kwa matumizi yako uwapo chuoni.

9. Unatakiwa kulipa kiasi cha fedha kama kilivyoambatanishwa na barua hii.

10. Hutapokelewa chuoni iwapo utafika bila kutekeleza vifungu vilivyotajwa hapo juu. Lipa mapema ili uweze kusajiliwa. Fedha ikishalipwa hairudishwi.

11. Nafasi yako itapotea kama utashindwa kuripoti wiki moja baada ya tarehe ya kufungua chuo.

……

ELIAS CHRISOSTOMS MSIGWA

KNY: MKUU WA CHUO.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO
YA UFUNDI STADI
CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI CHA WILAYA YA KWIMBA

I. MALIPO MBALIMBALI YA CHUO.

JEDWALI A: KARO NA MICHANGO MBALIMBALI.

Na	AINA YA MALIPO	GHARAMA KWA MWAKA		MUHULA WA KULIPA			
		Bweni	Kutwa	MUHULA WA I		MUHULA WA II	
				Bweni	Kutwa	Bweni	Kutwa
01	Karo (Ada) masomo	120,000/=	60,000/=	60,000/=	30,000/=	60,000/=	30,000/=
02	Fedha ya uchakavu	20,000/=	20,000/=	20,000/=	20,000/=		
03	Fedha ya Michezo	10,000/=	10,000/=	10,000/=	10,000/=		
04	Kitambulisho	5,000/=	5,000/=	5,000/=	5,000/=		
05	Nembo ya VETA	5,000/=	5,000/=	5,000/=	5,000/=		
06	Gharama za godoro	10,000/=		10,000/=			
07	Fedha ya Mtihani (Life Skills)	25,000/=	25,000			25,000/=	25,000/=
	JUMLA	**195,000/=**	**125,000/=**	**110,000/=**	**70,000/=**	**85,000/=**	**55,000/=**

ZINGATIA: Malipo haya utayalipa kwa namba ya malipo ya serikali (Control Number) utakayopewa na Chuo.

JEDWALI B: Malipo mengine kwa ajili ya huduma mbalimbali kwa mwanafunzi.

NA	MAHITAJI/HUDUMA	IDADI	GHARAMA/@	KIASI
01	Suruali za sare	02	25,000/=	50,000/=
02	Ovaroli moja	01	35,000/=	35,000/=
03	Fulana (T-Shirts)	02	15,000/=	30,000/=
04	Sweta (Sweater)	01	30,000/=	30,000/=
05	Bima ya Afya	Mwaka mmoja	50,400/=	50,400/=
	Jumla			**195,400/=**

ZINGATIA: Malipo haya yatalipwa moja kwa moja Chuoni utakapowasili, kwa ajili ya gharama za sare na Bima ya afya.

HIVYO: Jumla ya malipo yote, (JEDWALI A + JEDWALI B) ni,

TZS. 390,400/= (Mwanafunzi wa Bweni)

TZS. 320,400/= (mwanafunzi wa Kutwa)

II. MAHITAJI MENGINE.

1. Uje na **Mashati mawili (02) meupe ya mikono mifupi na kitambaa cha tetron.**
2. Uje na Viatu **Vyeusi, vya Ngozi vyenye visigino vifupi na vya kufunga na gidamu** – Jozi moja.
3. Uje na **viatu vya usalama kwenye karakana (Safety Boot) vyeusi** – Jozi moja
4. Uje na Soksi jozi mbili **(Nyeusi kwa wavulana, na Nyeupe kwa Wasichana)**
5. Uje na **"Track suit" 01, rangi ya blue bahari, na viatu vya michezo**, kwa ajili ya michezo,
6. Uje na **Shuka mbili, rangi ya bluu na pinki/blanketi jepesi, na mto mmoja wa kulalia.**
7. Uje na **chandarua (Size 3x6)** kwa ajili ya kujikinga na mbu.
8. Uje na **ndoo mbili ndogo** kwa ajili ya kuhifadhia maji na kuogea.
9. Uje na vyombo vya chakula **(Sahani 1, Bakuli 1, Kikombe, na kijiko)**
10. Uje na madaftari ya masomo **NANE (Counter Books Quire 3)**
11. Uje na "Mathematical Set" – Moja
12. Uje na Kikokotozi cha Mahesabu (Scientific Calculator) – Moja
13. Uje na Bunda moja la karatasi **(Ream paper – A4) – Ream Moja (Double A** au **MAPACHA Vv)**
14. Uje na **Jembe jipya lenye mpini** – Jembe moja
15. Uje na **Panga** au **Fyekeo** – Moja
16. Uje na picha za **"Passport size" nne (4) zenye "Background" ya blue na zilizopigwa hivi karibuni.**
17. Uje na faili moja kwa ajili ya kuhifdhia nyaraka zako binafsi, (Box File)

III. MAELEKEZO YA KUZINGATIA.

1. **<u>UTARATIBU WA MALIPO:</u>**
   Ada inawezekana kulipwa kwa awamu mbili, kulingana na mihula ya masomo (Muhula wa Kwanza – mwanafunzi anaporipoti chuoni, na Muhula wa Pili – Julai, 2024).
   <u>NAMNA YA KULIPA</u>: Mwanafunzi atapewa Namba ya malipo ya serikali "Control Number" ya kulipia ADA na michango ya Jedwali A, na atakuja na risiti inayoonyesha malipo aliyolipa.
2. **<u>BIMA YA AFYA</u>**:
   Kila mwanafunzi atalazimika kuwa na BIMA YA AFYA ya NHIF. Endapo mwanafunzi ni mnufaika wa BIMA YA AFYA kutoka nyumbani, aje na kadi yake. ***Mwanafunzi asiye na Bima ya Afya na hajalipia, hatapokelewa.***
3. **<u>ADA ZA MITIHANI:</u>**
   Wanafunzi watakaofanya vizuri katika masomo yao na kufikia viwango/sifa za ufaulu, wataruhusiwa kufanya mtihani wa Taifa "Competence Based Assessment" [CBA], na watapaswa kulipia mtihani huo. Wazazi/walezi watapewa taarifa ya kiasi cha ADA ya Mtihani katika taarifa za wanafunzi wakati wa likizo ndefu ya June/Julai, 2024.
4. **<u>KUPOKELEWA</u>**:
   Waliolipa Ada, na kutimiza masharti yote, ya michango na vifaa vilivyoainishwa kwenye maelekezo, **<u>ndio watakaopokelewa Chuoni</u>**. Utapaswa kuonyesha vitu vyote ulivyoagizwa kwa Walimu katika dawati la kusajiliwa Chuoni utakaporipoti na utapewa kibali ili upokelewe katika FANI yako na BWENINI.

VET MED FORM - IE

VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY (VETA)

MEDICAL EXAMINATION FORM

15/12/2024

The Medical Officer

Government Hospital/Health Centre/Dispensary,

.....

.....

.....

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION:

NAME: ……..

Please examine the above named trainee to certify his/her fitness to undergo training and subsequently work as a/an ……

i. Eyesight:……

ii. Hearing:……..

iii. Asthma:……..

iv. Epilepsy:……

v. Other serious diseases:……..

MEDICAL CERTIFICATE:

I have examined the above named trainee and consider that he/she is pysically fit/unfit for training as above:

Date:…… Designation:…… Signature & Official stamp:……

KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

MWANACHUO.

Mimi.....ninakubali nafasi ya mafunzo katika fani niliyopangiwa na nitazingatia sheria na kanuni za chuo.
Sahihi·····Tarehe ·····

MDHAMINI

Mimi ·····S.L.P ····· Ninathibitisha kuwa ninamdhamini ····· Na nitalimlipia gharama zote za mafunzo (ada) pamoja na nauli wakati wote wa kwenda chuoni nakurudi nyumbani kwa likizo na baada ya mafunzo.

Sahihi·····Tarehe ·····

SHERIA ZA CHUO KWA WANAFUNZI WA KUTWA NA BWENI:

ILI KUFANIKISHA MAFUNZO YA UFUNDI KILA MWANAFUNZI ANATAKIWA KUFUATA SHERIA ZIFUATAZO:

1. MAHUDHURIO:

[a] Kila mwanafunzi anatakiwa kufika chuoni kabla ya saa 1:30 asubuhi. Hii ina maana ifikapo saa 1:30 wanafunzi wote wawe wameshafika chuoni . Adhabu kali itatolewa kwa wachelewaji.

[b] Mwanafunzi hatakiwi kutoka nje ya chuo kwenda nyumbani ,hospitali au sehemu nyingine yoyote ile bila ya kuruhusiwa na mwalimu wa zamu/mwalimu wa darasa/Matron/Warden na Msajili. Hivyo wakati wa kutoka mwanafunzi sharti awe na kibali (gate pass) ya kutoka nje ya chuo iliyosainiwa na walezi tajwa.

[c] Mwanafunzi apatapo matatizo ya msiba,kuuguliwa au kuugua mwenyewe ni lazima habari/taarifa zifike chuoni , bila ya kufanya hivo ni kosa na kwamba adhabu kali itatolewa ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo au kufukuzwa chuo.

[d] Mahudhurio chini ya asilimia 85% ya masomo yatapelekea mwanafunzi kunyimwa cheti cha kuhitimu.

2. MAVAZI

[a] Sare za chuo ni suruali ya Blue na shati jeupe mikono mifupi na fulana t-shirt. Sare hiyo ivaliwe wakati wote mwanafunzi awapo chuoni na wakati wa safari ya kuja chuoni na kurudi nyumbani. Wakati wote shati liwe limechomekewa.

[b] Ovaroli livaliwe wakati wa vipindi vya mafunzo ya vitendo na kazi za mikono tu.

[c] Viatu vyenye visigino virefu na kandambili au viatu vya wazi [sandals] haviruhusiwi kuvaliwa darasani au kwenye karakana.

3. USAFI WA MWILI

[a] Hairuhusiwi kuvaa hereni, pete, bangili, mkufu na mapambo ya aina yoyote ile kwa kipindi chote cha mafunzo.Hairuhusiwi kutumia vipodozi au manukato yanayotoa harufu kali .

[b]Nywele kwa wavulana

[i] zikatwe ziwe fupi sana, KIPARA hakiruhusiwi kabisa.

[ii] Ndevu haziruhusiwi

[c]Nywele kwa wasichana

[i] Zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mistari ya kurudi nyuma.

[c] Kucha zisifugwe kabisa wala kupakwa rangi.

4. WIZI WA MALI ZA CHUO AU MALI BINAFSI

[a] Vitendo vyovyote vya wizi haviruhusiwi na kwamba ikibainika mwanafunzi ameiba mali ya chuo au ya mwanafunzi mwenzake , atafukuzwa chuo mara moja.

[b]Ukipoteza kifaa cha chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya kifaa kwa kukinunua au kukileta.

[c] Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyoko ndani ya chuo.

[d] Mwanafunzi atapekuliwa wakati wa kutoka karakana au getini.

5. UGOMVI:

Matukio ya ugomvi, kupigana, na kushambuliana ni makosa ya jinai na kwamba atakayepatikana akijihusisha na matendo ya namna hiyo, atafukuzwa chuo mara moja.

6. ULEVI:

Mwanafunzi atakayebainika kuwa na tabia za ulevi, uvutaji sigara, bangi na mihadarati ya aina yoyote au kuonekana sehemu kama hizo, atafukuzwa chuo mara moja.

7. MAPENZI:

[a]Uhusiano wa kimapenzi chuoni kati ya mwanafunzi na mwanafunzi au kati ya mfanyakazi na mwanafunzi hauruhusiwi kabisa.

[b] Mwanafunzi wa kiume au wa kike haruhusiwi kuingia maeneo wanayoishi wafanyakazi wa chuo bila kibali au ruhusa.

(c)Wanafunzi wa kiume hawaruhusiwi kuingia bweni la wanafunzi wa kike hali kadhalika wanafunzi wa kike hawaruhusiwi kuingia bweni la wanafunzi wa kiume bila ruhusa na sababu maalumu.

8. MIGOMO NA UVUNJIFU WA AMANI:

Mwanafunzi atakayesababisha na kuchochea mgomo au uvunjifu wa amani chuoni atafukuzwa chuo bila kusita kwani ni kinyume na taratibu za chuo na nchi kwa ujumla.

9. LUGHA YA KUFUNDISHIA

Lugha inayotumika kufundishia masomo darasani ni kiingereza, hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi kujifunza kiingereza kukidhi mahitaji ya Mitaala ya VETA.

10. KUSAJILI MAJINA SAHIHI NA HALALI

Mwanafunzi atapaswa kusajili majina sahihi na halali kama yanavyoonekana kwenye vyeti vya kuzaliwa/shule ya msingi/ sekondari au chuo. Siyo ruhusa mwanafunzi kubadilisha jina bila hati maalumu ya kiapo kutoka Mahakamani kwa uthibitisho na taarifa kupelekwa kwa Mkuu wa Chuo mara moja.

11. MATUMIZI YA SIMU ZA KIGANJANI:

Mwanafunzi haruhusiwi kutumia simu wakati wa vipindi vya masomo darasani yaani kuanzia saa 1:30 asubuhi mpaka saa 8:30 mchana. Adhabu zitatolewa kwa mwanafunzi atakayekiuka kanuni hii ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo.

12. KULALA NJE YA CHUO:

Mwanafunzi wa **bweni** haruhusiwi kulala nje ya chuo bila ruhusa kutoka kwa Mkuu wa chuo na kwamba atakayekiuka kanuni hii atafukuzwa chuo bila kusita.

13. SIKU ZA KUTOKA NJE YA CHUO:

Mwanachuo wa **bweni** ataruhusiwa kutoka nje ya chuo akiwa amevaa sare (uniform) za chuo siku zifuatazo tuu!:

(i) Jumamosi saa 12.00 asubuhi hadi saa 12.00 jioni

(ii)Jumapili saa 12.00 asubuhi hadi saa 12.00 jioni

Aidha wakati wa kutoka nje ya chuo mwanafunzi ataandika jina lake kwenye kitabu getini na atasaini wakati wa kurudi chuoni.

13. KITAMBULISHO CHA CHUO

Mwanachuo yeyote anayeruhusiwa kutoka eneo la chuo anapaswa kuwa na kitambulisho cha chuo na atajiandikisha lango kuu akiwa amevaa sare ya chuo.Mwanafunzi atakayeonekana nje ya maeneo ya chuo bila kuwa na kitambulisho atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa nafasi ya kulala bwenini au kufukuzwa Chuo.

15. KUPIKA NA KULA BWENINI

Mwanafunzi haruhusiwi kupika au kula chakula bwenini na kwamba si ruhusa kuwa na vifaa vya kupikia au kuchemshia maji vya aina yoyote ile. Atakayekiuka kanuni hii atatolewa bwenini au kufukuzwa chuo.

16. MATUMIZI YA UMEME NA MAJI

Mwanafunzi atapaswa kutumia umeme na maji kwa matumizi sahihi na kwamba mwanafunzi wa **bweni** atapaswa kuzima taa darasani, bwenini na bwaloni ifikapo saa 4.00 za usiku na siyo vinginevyo. Adhabu kali itatolewa kwa atakayekiuka kanuni hii.

17. WAGENI:

Mwanafunzi wa **bweni** haruhusiwi kumkaribisha/ kutembelewa na mgeni bwenini, darasani au bwaloni na kwamba wageni wote watafikia ofisi ya mapokezi na kuelekezwa utaratibu wa kuonana na mwanafunzi. Adhabu kali itatolewa kwa atakayekiuka kanuni hii. Aidha mwanafunzi wa **bweni** atatembelewa na mzazi/ mlezi au ndugu kwa siku za:

(a) Jumamosi kuanzia saa 7.00 mchana mpaka saa 12.00 jioni.
(b) Jumapili na siku za sikukuu kuanzia saa 7:00 mchana mpaka 12.00 jioni.

18. MATUMIZI YA MADARASA NA SAMANI:

Mwanafunzi atatumia vyumba/madarasa na vifaa kufuatana na shughuli zake na kwamba siyo ruhusa kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya chuo. Adhabu kali itatolewa kwa atakayekiuka agizo hili.

19. ITIKADI ZA KISIASA:

Mwanafunzi haruhusiwi kuonyesha kuwa mkereketwa au mfurukutwa wa chama chochote cha siasa awapo chuoni na kwamba hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa kwa atakayebainika kufanya siasa katika eneo la chuo.

20. ITIKADI ZA DINI:

Chuo cha VETA Mwanza hakiendeshwi kwa itikadi ya Dini yoyote, hivyo masuala yote yanayohusu imani za Dini mbalimbali hayataratibiwa na chuo na kwamba mwanafunzi atakayesabisha uvunjifu wa amani kwa sababu za udini atachukuliwa hatua kali za nidhamu.

MWISHO:

Nakupongeza tena kwa kuchaguliwa kujiunga na mafunzo ya ufundi stadi katika chuo cha VETA Mwanza. **"Karibu sana".**